

UGONJWA WA KIDELI (Newcastle Disease)

Na Augustino chengula

DALILI ZA UGONJWA WA KIDELI

Dalili za ugonjwa wa kideli hutegemea sana eneo ambalo kirusi atakuwa ameshambulia. Dalili zaweza kuonekana katika mfumo wa upumuaji, chakula, fahamu na maeneo mengine kama yanayozunguka macho na shingo. Ugonjwa huanza kwa haraka na dalili huanza kuonekana kwa pamoja ndani ya banda kuanzia siku 2 hadi 12 tangu virusi viwapate kuku (wastani siku 5). Kuku wadogo hupata ugonjwa huu kirahisi zaidi na hata dalili huanza mapema kwao ukilinganisha na wakubwa.

1. Dalili za mfumo wa upumuaji:

- kuku hupiga chafya
- kuku hutweta kwa ajiri ya kuvuta hewa kwa nguvu
- kutokwa na mafua
- kukohoa
- hupumua kwa sauti ya mkwaruzo au yenye makelele

Picha



Kuku wote wawili hapa juu wanaonyesha kupumua kwa shida kwasabu ya njia ya
hewa kuziba na ute mzito wa makamasi.

Akipasuliwa:

- Utakuta makamasi ndani ya koromeo yaliyojaa kuzuia upumuaji
- Mara chache unaweza kukuta damu kwenye ukuta wa koromeo
- Ndani ya pua huwa na makamasi

2. Dalili za mfumo wa chakula:

-Muhalo wa majimaji wenyе rangi ya kijani

-Kutokwa na ute mdomoni

-Kukosa hamu ya kula



Kutoka ute mdomoni

Akipasuliwa:

-utumbo huwa na rangi ya damu ya mzee au uzambarau mwekundu

-Damu huonekana kwenye firigis na hasa maeneo ya shingo ya firigis

Picha



Cornell University/PIADC

Utumbo wenyе damu baadhi ya maeneo





Firigisi zenyе damu hasа sehemu ya shingo

3. Dalili za mfumo wa fahamu:

- Kunyong'onyea/unyogovu
- Kutetemeka misuli
- Mabawa kulegea
- kutembea huku akiburuza miguu
- Kujinyonga shingo kwa kuzungusha kichwa
- Kujizungusha katika umbo la mduara
- Mpapatiko wa kudumu kwa kuku waliotabaani
- Kupooza mwili mzima

Picha





Kuku hawa wakiwa katika maumbo tofautitofauti ya kupooza mwili, watatu wa kwanza wanaonyesha kujinyonga kwa shingo na kuzungusha kichwa, wakati huyu wa mwisho kapooza mwili mzima.

Akipasuliwa:

-Mifumo ya fahamu huwa imevimba

4. Mfumo wa utagaji mayai:

-Kushuka kwa utagaji wa mayai hadi kufikia kiwango cha kutotaga kabisa

-Mayai huwa na rangi, umbo na sura isiyo ya kawaida

-Ngozi ya ganda la yai kuwa nyembamba

-Ndani huwa na majimaji (tepetepe)



Dr. Jaime Ruiz

Yai la kushoto zima na la kulia limekuwa jeupe sana lenye ngozi laini



poultrykeeper.com

Mayai yenye ngozi nyembamba inayobonyea kirahisi na ngozi yake ni nyeupe

5. Dalili nyingine:

- Vifo nya gafla
- Ugonjwa huweza kuwapata kuku wote ndani ya banda kwa wakati mmoja
- Kuku wadogo waweza kufa wote lakini hata wakubwa waweza kufa kwa asilimia 100 ndani ya banda
- Kuvimba maeneo ya shingo na kuzunguka macho



Jicho jekundu lililojaa damu na limevimbba

Matibabu

- Ugonjwa wa Kideli hauna dawa
- Kinga ya kuzuia ugonjwa huu ni kuchanja kuku kwa wakati unaotakiwa (soma **hapo juu**)